MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 7 TOLEO 25

FEBRUARI 4 , 2009

KIJARIDA CHA BURE— CHAPA NAKALA; MPE MWINGINE—USIBANIE!

KASHFA YA RADA

CHENGE NA DR.IDRIS WANANGOJEA NINI?

Na. Fred Katunzi



Ile kashfa ya rada imeanza kupata uhai mpya baada ya taarifa kuwa kesi dhidi ya wahusika wakubwa imeiva na sasa idhini imetolewa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuleta mashtaka dhidi ya wahusika.

Miongoni mwa wahusika ambao tayari kijarida chako kiliwahi kuzungumzia miezi kadhaa iliyopita ni pamoja na dalali Shailesh Vithlani na swahiba wake na mshirika wa kibiashara ambaye pia ni mfadhili mkubwa wa CCM Bw. Tamil Somaiya.



Mkurugenzi wa Tanesco Dr. Idris Rashidi (Kushoto) na Mbunge wa Bariadi Mashariki Mhe. Andrew Chenge

Kwa upande wa watumishi wa serikali vinara wanaotuhumiwa ni pamoja na aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wakati wa mradi huo ambaye sasa ni Mbunge wa CCM Bw. Andrew Chenge pamoja na aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ambaye Dr. Idris Rashid ambaye sasa hivi ni Mkurugenzi wa Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO). **(Inaendelea Uk. 2)**



Benjamin. G. Mwalukasa

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimerushusiwa!**

HOJA YA MWANAKIJIJI — MIAKA 32 YA CCM!

Kesho ni miaka 32 kamili tangu kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi tarehe 5/2/1977. Chama hicho kilipozaliwa kilikuwa kimejita kuwa ni chama cha Mapinduzi na kurithi malengo na misingi ya TANU na ASP vyama ambavyo vilikuwa vimeshika hatamu ya uongozi Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya mwaka 1977 iliyotangaza kuvunjwa kwa TANU na ASP na kuundwa kwa CCM chama hicho basi kilitakiwa kiwe "cha kuendeleza mapinduzi ya kijamaa nchini Tanzania na Mapambano ya Ukombozi wa Afrika"

Zaidi ya yote Katiba hiyo ya CCM Inasema kuwa chama hicho "tunataka kiwe chombo madhubuti katika muundo wake na hasa katika fikra zake na vitendo vyake vya kimapinduzi vya kufutilia mbali aina zote za unyonyaji nchini, na kupambana na jaribio lolote lile la mtu kumuonea mtu au shirika au chombo cha nchi kuonea na **(Inaendelea Uk. 2)**

Ndani ya Toleo Hili

Kashfa ya Rada	1, 2
Hoja: Miaka 32 ya CCM	1,3
Jessy: Wabakaji nao vipi?	3
Dr. Slaa: Juu ya Rada	4
Hoja ya Nguvu	5
Dr. Mwinyi aliongopa?	5
Picha na Katuni	6

HATIMA YA DR. IDRIS NA MHE. CHENGE

Licha ya uzito wa tuhuma zilizo mbele zao watumishi hao bado wanaendelea na kazi zao kama kawaida.

Uchunguzi wa Taasisi ya Uingereza inayohusiana na Makosa Makubwa ya Ulaghai (Serious Fraud Office—SFO) imekusanya ushahidi wa kutosha dhidi yao ushahidi ambao tunaamini endapo tungekuwa na utamaduni wa kupima uzito wa tuhuma basi viongozi wabovu wangekuwa wanawajibishwa mapema zaidi.

Karika barua ambayo imekuwa ikinukuliwa na vyombo vya habari ambayo nakala yake tunayo (unaweza kuisoma barua hiyo kwenye tovuti yetu ya http://www.mwanakijiji.com) Taasisi hiyo ya Uingereza inasema pasipo utata wote kuhusu Chenge kuwa ni mhusika kinara katika kile kinachoaminiwa malipo ya rushwa yaliyosababisha yeye kuandika maoni ya kisheria ambayo yalichangia ununuzi wa rada hiyo katika bei ya kuruka.

Katika barua hiyo ya tarehe 21 Machi, 2008 iliyotumwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Tanzania Afisa wa SFO ambaye anasimamia uchunguzi huo Bw. Matthew Cowie ametaja watu na taasisi tisa ambao walitaka kuwachunguza kutokana na uzito wa ushahidhi dhidi yao.

Kwa upande wa Tanzania wahusika ni hao watatu. Tulishaandika kwenye matoleo yetu ya nyuma kuhusu Shailesh Vithlani na Tamil Somaiya.

Bw. Cowie anasema kuwa "kuna sababu ya kutosha kuamini kuwa wote waliotajwa hapo juu wamefanya makosa ya kifisadi kwa mujibu wa kifungu 1 cha Sheria ya Kuzuia Rushwa ya 1996 (hii ni sheria ya Uingereza ikifanyia mabadiliko sheria nyingine—Mhariri). "

Kwa mujibu wa sheria hiyo adhabu ya juu kabisa ya watakaokutwa na hatia ni kifungo cha miaka saba jela. Taasisi hiyo ilitambua pia uchunguzi uliokuwa unafanywa na taasisi yetu ya TAKUKURU na habari zote tulizozipata kutoka vyanzo vyetu Uingereza zinasema kuwa TAKUKURU imepewa msaada wote na ushahidi wote dhidi ya Chenge na wenzake na maafisa wengine ambao majina yao bado hayajatwa hadharani kuhusiana na rada.

Kwa mujibu wa barua hiyo dalali ambaye amekuwa akihusishwa na mikataba mingine ya kifisadi kwa niaba ya makampuni mbalimbali na serikali ya Tanzania Bw. Vithlani "alikuwa na jukumu la kuwalipa maafisa wa umma ambao walikuwa na ushawishi katika suala la ununuzi wa rada".

Taasisi hiyo inasema pasipo shaka yoyote kuwa "Andrew Chenge Mwanasheria Mkuu alikuwa ni mmoja wa watu muhimu zaidi ambao bila ya shaka Vithlani alitarajiwa kumlipa."



Barua hiyo inaelezea kwa kirefu maamuzi mbalimbali ambayo Chenge aliyachukua ambayo kwa pamoja yalifanikisha Taifa kuingia hasara ya mabilioni ya shilingi. Ripoti hiyo inasema "Kwa kuchukua uamuzi huu, Chenge alikuwa anaweka maslahi ya kiuchumi ya Tanzania mashakani".

Kwa maneno mengine, Andrew Chenge mtu aliyepewa dhamana ya kusimamia Sheria zetu anadaiwa kuwa ni mtu wa kwanza kuzivunja kwa kuweka maslahi yake na ya rafiki zake mbele kuliko yale ya Taifa.

Licha ya kutakiwa na benki yake ya Barclay kuelezea chanzo cha mapato yake hayo makubwa Bw. Chenge alishindwa kufanya hivyo hata kumlazimu kuvunja uhusiano wake na benki hiyo.

Barua hiyo inasema kuwa hadi mwaka 2006 akaunti za Chenge na Mkewe zilikuwa zimefikia Paundi 804,000!

Kinachoshtua zaidi ni kuwa Chenge akiwa ni Mwanasheria Mkuu alitakiwa kutangaza mali zake zote kwa tume ya maadili na hakufanya hivyo. Hiyo ni kwa mujibu wa sheria ya maadili ya mwaka 1995. Hili limethibitishwa na TAKUKURU.

Licha ya hili kujulikana Chenge aliendelea kuwa Mwanasheria Mkuu wa Tanzania kwa karibu miaka 11.

Mwezi Mei 1998 malipo ya Dola 600,000 yalifanyika toka akaunti ya ya Chenge kwenda kwenye akauni ya Langley Investments Ltd. Kampuni hiyo ilikuwa inamilikiwa na Idriss Rashid ambaye kwa mujibu wa barua ya SFO alikuwa ndiye Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa mujibu wa SFO, Bw. Rashid alikuwa ni mtu mwingine muhimu katika majadiliano ya kusaini mkataba wa ununuzi wa rada hiyo.

Ripoti hiyo inasema kuwa "(Dr. Idris) alikuwa ni mtu muhimu sana katika majadilano ya kulipia rada hiyo ambapo pasipo hayo ununuzi wa rada usingefanyika."

Kiasi ambacho Dr. Rashid alikipokea kwenye akaunti yake tumethibitishiwa pia na vyanzo vyetu vya ndani serikali kuwa nacho hakikutangazwa kwa tume ya maadili ya viongozi.

Sheria ya maadili ya Umma ya 1995 inmeziweka nafasi za Bw. Chenge na Dr. Idris kuwa ni miongoni ya zinazotakiwa kutoa taarifa ya utajiri na mali zao kwa Kamishna wa Maadili. Kipengele cha 9 na cha 23 cha Ibara ya 4 kinataja nafasi hizo kuwa ni za viongozi wa umma. Hivyo kutokutimisha masharti hayo ni kuvunja sheria hiyo.

Tunaamini ya kuwa tuhuma dhidi ya watumishi wa umma zinapokuwa nzito basi ni wajibu wa hatua kuchukuliwa dhidi yao au wao wenyewe "kupima" uzito wa tuhuma hizo dhidi yao na kuamua kuchukua hatua za kujiuzulu.

Na katika kujiuzulu haja ipo na ya lazima ya kubadilisha sheria ya maadili pamoja na sheria nyingine ili mtu anayejiuzulu asilipwe mafao yoyote yale yanayohusiana na wadhifa aliokuwa ameushikilia.

Unaweza kusoma barua nzima ya SFO kwa Mwanasheria Mkuu kwenye tovuti yetu ya mwanakijiji.com sehemu ya Vielelezo na Ushahidi.

Tunatumaini tuhuma dhidi ya Chenge na Dr. Idris ni nzito mno kiasi kwamba hawastahili nyadhifa zao. Tuanze hapo.

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

HOJA YA MWANAKIJIJI

MIAKA 32 YA CCM

kudhalilisha wananchi, kudhoofisha uchumi au kuzorotesha maendeleo ya Taifa"

Miaka 32 baadaye tunajiuliza kama kweli CCM chama kilicholeta matumaini kwa mamilioni ya watu wetu kimeweza kweli kusimamia misingi ya kuundwa kwake? Je leo hii kuna watu wanaoonea watu wengine? Je leo kuna chombo ambacho kinaonea, kudhoofisha au hata kuzorotesha maendeleo ya taifa? Je ni kweli chama hiki bado ni madhubuti katika muundo wake na hasa kwenye "fikra na vitendo vyake vya kimapinduzi"?

Chama cha Mapinduzi kimeandika historia katika Taifa letu, historia ambayo haiwezi kufutwa kamwe. Hata hivyo ninaamini kama nilivyoandika kwenye gazeti la Tanzania Daima la leo kuwa kama Tanzania inataka kuwa na nafasi ya kupiga hatua ya haraka ya maendeleo tena kwa muda mfupi ni lazima mabadiliko makubwa yatokee kwenye Chama cha Mapinduzi kuliko mahali pengine popote. Katika makala yangu nimefafanua ni mabadiliko ya aina gani hayo.

Historia bado inaendelea kuandikwa na muamuzi wa kweli ni muda. Dalili zote zilivyo hata hivyo zinaonesha kuwa labda tungekuwa bora zaidi kama TANU na ASP visingekufa!

Hali yetu ya leo hii ambayo tunatakiwa tuamini kuwa "tumeendelea" na ya kuwa "kuna tofauti kubwa" kuliko huko nyuma ni matokeo ya moja kwa moja ya utawala wa CCM.

Jiulize hata hivyo kama wafadhili wakisitisha misaada isiyo ya lazima, kama tukipunguza kuagiza bidhaa ndogondogo kutoka 'ng'ambo" ambazo zinaweza kuzalishwa nchini, na kuona wawekezaji wa kigeni wakipungua kwa ghafla je Tanzania itaendelea kuwa jinsi ilivyo? Je tunaweza kuwa na maisha tofauti bila wawekezaji wa kigeni, misaada ya mabilioni kutoka ng'ambo na kukinga bakuli letu la misaada huku tukicheka cheka na kujisifia? Tanzania hiyo inaonekanaje?

Miaka ya nguvu zake CCM ilipigia mbiu sera za kujitegemea. Leo hii hakuna kiongozi mwenye kuimba "kujitegemea" tena na sasa wamebakia kuendeleza sera za "Kujimegea".

Kama taarifa yetu kuu kuhusu kashfa ya rada inavyoonesha hatuna budi kujiuliza; Kama kwenye rada watu wawili tu wanaonekana kumegeana mamilioni ya fedha, je kwenye IPTL, Buzwagi, Richmond, n.k wamemegeana kiasi gani? Je kweli tunaweza kutengenesha CCM na ufisadi nchini?
Je CCM kweli ni kinyume na ufisadi?

DA'JESSY: WABAKAJI NAO WAUAWE!

Jessica L. Fundi



Namuunga mkono kwa asilimia 101 Waziri Mkuu Pinda kutaka wauaji wa Albino wakikamatwa nao wauawe papo hapo. Mfano aliotumia Waziri Mkuu ni mzuri. Kwamba ukimkuta mtu ameshika mkono na unavuja damu na ukaona anakimbia huku mtu Albino anamwagika damu na ukamkimbiza mtu yule basi ukimkamata hakuna haja ya ushahidi mwingine wala kwenda mahakamani bali mtu huyo auawe tu.

Nilipoufikiria na mimi naamini kuwa wakati umefika kwa kwa wabakaji wote nao kupata adhabu kama hiyo.

Vitendo vya kiubakaji ambavyo vimekuwa vikifanyika hadi kwa watoto wachanga humu nchini kwa muda mrefu vimefikia mahali pa viongozi wetu kusema "sasa tumechoshwa".

Fikiria kisa cha Mzee wa Vingunguti ambaye mwishoni mwa mwaka jana alipelekwa kizimbani kwa tuhuma za kubaka mtoto wa miaka minne.

Mzee huyo inadaiwa alidakwa na wananch na nusura wampe kipigo kikali. Bahati mbaya akaokolewa na kupelekwa mikononi mwa polisi.

Au wale vijana waliokamatwa kule Rukwa ambao walituhumiwa kumbaka mtoto wa shule ya msingi wa miaka 14 tena kwa zamu?

Au kisa cha yule kijana kule Bunda aliyembaka mtoto wa darasa la tano baada ya kumnyemelea akienda shule, kumkamata kwa nguvu na kumvutia nyumbani kwake. Kijana huyo baadaye amehukumiwa miaka 30 jela.

Kweli adhabu hiyo ya miaka 30 inatosha kwa unyama huu? Kwa mtu anayebaka kitoto kichanga na kukiharibu maumbile yake milele kweli kuna sababu ya kumpeleka mahakamani?

Mtu kama huyo akikutwa katika eneo la tukio kwanini tunahangaika kumpeleka Mahakamani?

Mimi namuomba sana Waziri wetu Mkuu mwenye huruma huruma ambayo tuliiona wiki iliyopita Bungeni, kuwa atuonee huruma na sisi kina dada, watoto wetu na dada zetu.
Kwamba atangaze mapema iwezekanavyo kuwa watuhumiwa wote wa ubakaji nao wakikutwa eneo la tukio na nguo zao au vingine "vinaning'inia" na wao wauliwe papo hapo ili liwe funzo kwa watu wengine.

Kina mama wa Tanzania tumechoshwa kuishi katika hofu na daima kuwa roho juu watoto wetu wanapoenda gengeni au shuleni. Tunawaisihi serikali hii sera mpya "jino kwa jino" ndiyo sera pekee inayowafaa wauaji wa Albino na wabakaji wa kina mama!

Tunaomba wabunge waliounga mkono msimamo wa Waziri Mkuu wasimame na wahesabiwe wakiunga mkono suala hili. Vinginevyo na sisi kina mama tutafanya maandamano nchini kuhamasisha mauaji ya wabaki wote kwani wamerundikana jela tu wakipoteza muda na fedha za taifa letu.

Soma bure

CHENGE NA IDRIS WASHITAKIWE—DR.SLAA

Na. Dr. Wilbroad Slaa



Nadhani sasa ni wakati wa kupiga kelele. Hili suala la rada limekaa muda mrefu. Watanzania hatujui kama kuna kitu kinaendelea. Taarifa zinazojitokeza zinazidi kutisha. Hadi hivi sasa tunajua mambo yafuatayo:

a)Taarifa ya SFO ya 21 Machi, 2008 yenye Ref. SPCQ!/D/MC iliyopelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikwisha kutoa mwelekeo mkubwa na kuonyesha maeneo yote yanayodhaniwa kuna sura nzito ya mashtaka ya kihalifu. Taarifa hiyo ya SFO ilionyesha wahusika wakubwa kuwa ni BAE Systems, Red Diamonds Trading Ltd and Merlin International Ltd, Envers Ltd, Tanil Kumar Chandulal Somaiya, Shailish Pragji Vithlani, and Andrew Chenge and others.

b) Taarifa hiyo iliweka wazi Kampuni aliyokuwa akitumia Chenge na Mke wake inayoitwa Franton International Ltd ambayo ilikuwa ikipokea fedha kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoka Frankfurt, Lichtenstein, na hatimaye kuingia Jersey, Uingereza. Kwa kitu kinachoonekana kama kupoteza dira.

c) Kampuni ya Franton International imepokea fedha kati ya June 1997 nadi April 1998 katika Akaunti ya US Dollars iliyoko Barclays Bank no 5966999.

d) Inaelekea Chenge mwenyewe alipohojiwa alikuwa akitoa kila mara maelezo ya kujikanganya, ikiwa ni pamoja na " yanatokana na "Professional Earnings", lakini hakuweza kuonyesha ni shughuli zipi za kitaalam zilizomwezesha kulipwa fedha hizo katika kipindi hicho (ambacho ni kipindi cha ununuzi wa Radar). Katika mazungumzo na J.O. Hambro mawakili wake alieleza kuwa inatokana na "family savings and Inheritance" (yaani akiba ya familia na urithi). Wenye akili watajiuliza hiyo akiba ya familia ni kutoka wapi na huo urithi ni kutoka wapi na kwa nani?

e) Tarehe 20 September, 1999 Chenge mwenyewe aliidhinisha kuhamisha kiasi cha GBP kutoka kampuni ya Fanton International kweny akaunti iliyoko Barclays kwenda Benki Royal Bank of Scotland International iliyoko Jersey. Mwaka 2006 alikabidhi mamlaka ya uendeshaji wa Akaunti hiyo kwa J.O.Hambro " kwa jina lake na la mkewe". Tarehe 13 Septemba, 2006 Fedha zilizokuwepo Benki zilimikiwa kwa mgawanyo wa asilimia 75% ikimilikiwa na Andrew Chenge na asilimia 25 ikimilikiwa na "Mrs Chenge".

f) Maelezo aliyotoa Chenge ndiyo inayoonyesha sura halisi ya ufisadi mkubwa uliokuwepo. Wapelelezi wanasema,

"We did have a P.O.Box for him in Dar, but... nothing should be sent to that address from Jersey, if Mr. C's government were to be made aware of these assets in London, they may confiscatethem notwithstanding they legally belonged to Chenge and were not obtained via 'brown envolopes..'He asked his financial advisers to send all documentation to C/o 11 Sidmouth, Rd, London."

> ***Mhe. Chenge amevunja Sheria ya Maadili kwa kutokutanga fedha zake za nje!***

f) Isitoshe, Mei1998 Mr. Chenge alihamisha fedha toka account yake kwenda Langley Investments Ltd (Langley), akaunti iliyokuwa ikisimamiwa (controlled) na Mr. Idriss Rashid (Rashid) - Itakumbukwa kuwa Dr. Rashidi alikuwa Gavana wa BOT kati ya Mwaka 1993 hadi 1998 katika kipindi muhimu cha majadiliano ya ununuzi wa Rada husika.

Kutokana na hayo yote basi:
i) Ni dhahiri kuwa kuna sheria nyingi za Tanzania zimevunjwa, na hatuoni sababu ya Serikali ya kuwa na kigugumizi katika kumfikisha Mr. Chenge, na Bwana Rashid katika vyombo vya Dola, na hasa Mahakamani ili hatima ya Rasilimali za Taifa zilizotumika vibaya katika ununuzi wa Radar ijulikane. Hatuwezi kuendelea kupiga kelele za nchi maskini wakati rasilimali za Taifa hili zinawaneemesha wachache.

ii) Mhe Chenge ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Uchunguzi umedhihirisha wazi kuwa Mr. Chenge, kama Mbunge hakutangaza Mali zake zilizokuwa Jersey na nje ya Nchi kama anavyotakiwa na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, 1995, kwa Kamishna wa Maadili.

Hii inaeleza wazi kwanini Kamishna wa Maadili aliwakataza viongozi wa Vyama vya Siasa kukagua Register ya maadili na kuweka masharti magumu. Kwa kitendo hiki, bila kesi mahakamani, Kamishna anatakiwa kutoa Taarifa kwa Mamlaka husika mara moja kuwa Mheshimiwa Chenge amevunja Sheria ya Maadili kwa kutokutangaza mali zake, na hivyo "automatically" amepoteza Sifa ya kuwa Mbunge.

Inashangaza kuwa Sheria hiyo nayo imepindishwa kwa makusudi kumlinda Bwana Chenge. Tukumbuke kuwa wakati sheria hiyo inatungwa na mabadiliko ya baadaye ni Chenge aliyekuwa Mwanasheria Mkuu? Je Ni nini au kuna nini nyuma ya kulindana huku?

g) Jambo hili la kutochukuliwa hatua stahiki na Kamishna wa Maadili linafanya zoezi la kujaza fomu za mali kuwa kichekesho pale hatua stahiki zinapokuwa hazichukuliwi na sheria zimevunjwa/ kukiukwa.

Mambo haya yanahusu Maslahi ya umma, na hata DPP wala Mwanasheria Mkuu hawawezi kuyanyamazia. Kwanza hadi sasa hakuna anayejua kitu gani kinaendelea. Hatutaki kuingilia kesi, lakini angalau basi Watanzania kama wenye mali wanatakiwa kujulishwa kama kuna uchunguzi wa ndani unaendelea, maandalizi ya kesi yamefikia hatu gani nakadhalika.

Hakuna mwenye hati miliki ya nchi hii, wote tuna haki yakujua kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. Pili, mjadala husika utaisukuma serikali kuharakisha uchunguzi kama bado haujakamilika. Tatu kama kuna mtu anakuwa analindwa wajue kuwa tunajua mengi na kuwa hakuna tena linaloweza kufichwa.

Kama lolote, atakayejaribu kuficha bomu litamlipukia kwa namna ambayo hajawahi kuiona. Nne mwenye kufahamu mengine zaidi naye tunaomba atumegee ili wote tusogee mbele kwa pamoja kwa maslahi ya nchi yetu.

Dr. Wilbroad Slaa (CHADEMA) ni Mbunge wa Jimbo la Karatu na Katibu Mkuu wa chama hicho.

HOJA YA NGUVU
TUSIKUBALI SERIKALI IIDHINISHE MAUAJI NJE YA SHERIA

Na. Ben Mwalukasa

Tumeshuhudia kitu cha ajabu Bungeni wiki iliyopita na tumeendelea kushuhudia vitu vingine vya kushangaza kwenye serikali hadi tumeonesha dalili ya kuvizoea. Tumefika mahali pa kuzoea ubovu kiasi kwamba wema ukisimamishwa mbele zetu hatuutambui. Inashangaza uovu unatukuzwa na wema unabezwa!

Kiongozi wa upinzani Bungeni ametoa tuhuma nzito sana dhidi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. Tuhuma ambazo hazijajibiwa hadi sasa na badala yake tumechezewa hisia zetu na vionjo vyetu kiasi kwamba tumeamua kufumbia macho uzito wa tuhuma hizo.

Kimsingi Mbunge wa Wawi Mhe. Hamad Rashid amemtuhumu Waziri Mkuu kutumia nafasi yake kama Waziri Mkuu kutoa maagizo ya mauaji na kinga kwa wavunja sheria kwa kisingizio cha kupambana na mauaji ya Albino nchini. Bw. Hamad amedai kuwa kwa Waziri Mkuu aliyeapa kuilinda, kuitetea na kuihafadhi Katiba ya Jamhuri ya Muungano kusimama na kusema maneno haya "Mkimuona mtu akamkata mwingine shingo naye muueni papo hapo kwani sasa viongozi wote tumechoka".

Sasa kwa watu wengine hilo siyo jambo



kubwa lakini wameshindwa kuelewa uzito wake. Waziri Mkuu anazungumza kwa niaba ya serikali. Hivyo mtu akisema "Serikali imesema kuwa wananchi wakimuona mtu akimkata shingo mwingine basi mtu huyo auawe papo hapo". Sasa watu wanasema "Pinda kasema". Ukweli ni kuwa siyo Pinda kama Pinda bali Pinda kama Waziri Mkuu na kwa maana hiyo msimamo wa serikali ni kuwa wauaji wa Albino wakikutwa au kushukiwa ndiyo wahusika basi wauawe papo hapo!

Hizo ni shutuma na tuhuma nzito sana dhidi ya serikali. Ndicho kiini cha swali la Mhe. Hamad. Kwamba, kama serikali iliyoundwa kwa mujibu wa sheria, serikali ambayo inatakiwa kuongozwa kwa sheria, serikali ambayo mara zote imetukatalia sisi wengine kuchukua sheria mikononi ya kuwa mshitaki, hakimu na mtoa adhabu, iweje leo serikali hiyo hiyo itangaze adhabu kwa watu ambao hawajafikishwa mahakamani?

Jibu lake ni kuwa wengi tumeyapokea maneno ya Waziri Mkuu kutoka kwenye hazina ya hisia na kilindi cha vionjo. Chozi lake lililomwaga limewayeyusha hata majasiri wa hoja. Watu wakapigwa bumbuwazi na mioyo yao ikaloa! Wakaacha kufikiri na wao sheria ikatupwa pembeni kwa huruma! Je tuvunje sheria kwa sababu tunajisikia uchungu na tunaumizwa?

Wasomaji wetu wa kwenye tovuti ya mwanakijiji.com asilimia 60.8 wanakubaliana na watu wachukue sheria mikononi kama alivyoagiza Waziri Mkuu, asilimia 34 hawakubaliani, na asilimia 5.2 hawajali lolote. Katika demokrasia tunaambiwa kuwa "wengi wape". Kama kwa namna yoyote utafiti (ambao si wa kisayansi hasa) unawakilisha mawazo ya Watanzania basi kinachosubiriwa sasa ni utekelezaji tu kwani Serikali imeshatoa kinga kwa wale watakaoua "wanaoua" albino.


Wabunge wana haki ya kujua kama wauaji wa watuhumiwa wa mauaji ya Albino wamepewa kinga ya mashtaka.

UHUSIANO NA IRAN: DR. MWINYI ALIFICHA NINI?

Na. Mahmoud Rashid

Imeripotiwa siku chache zilizopita na gazeti la Habari Leo la tarehe 30 Januari, 2009 kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dr. Hussein Mwinyi amesema kuwa mazungumzo aliyoyafanya alipokuwa Irani mwishoni mwa mwaka jana yalikuwa yanahusu ushirikiano kati ya nchi hizi mbili katika nyanja za kilimo na ufugaji kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.

Habari hizo hata hivyo zinaonekana kupingana na habari zilizotolewa na vyombo vya Iran na vyombo vingine vya kimataifa baada ya kutiwa saini makubaliano ya ushirikiano. Shirika la Xinhua la Uchina (lenye mwakilishi Tehran) liliripoti tarehe 21 January 2009 kuwa Tanzania imetia sahihi makubaliano ya ushirikiano wa kijeshi na Iran; makubali-



ano ambayo yalitiwa sahihi na Waziri wa Ulinzi wa Iran Bw. Mustafa Mohammed Najjar na Waziri wa Ulinzi na JKT wa Tanzania Dr. Hussein Mwinyi. Xinhua ilikuwa inanukuu habari kutoka chombo cha habari cha Wanafunzi wa Iran ISNA. "Baada ya kukaribishwa na Najjar, Mwinyi akiongoza ujumbe wa kijeshi aliwasili Tehran Jumatatu tayari kwa mazungumzo na maafisa wa Iran kuhusu Ushirikiano wa Ulinzi na Iran" liliripoti Xinhua.

Kwa mujibu wa Shirika huru la Habari la FARS la Iran lililoripoti juu ya makubaliano hayo "kushirikiana uzoefu wa kiulinzi na kijeshi, pamoja na kubadilishana wataalamu katika mambo ya ufundi na mafunzi ndiyo msingi hasa wa yaliyomo katika makubaliano hayo".

Shirika hilo lilitoa habari kuwa "mwanzoni (mwa mazungumzo) Iran ilisema utayari wake wa kuipatia Tanzania teknolojia ya kijeshi".

Yote haya yanatufanya tujiulize ni kitu gani hasa ambacho Dr. Mwinyi anajaribu kuficha. Suala la kilimo na ufugaji haliko chini ya Wizara yake na ya kuwa ujumbe ulioenda Tehrani haukuwa kutoka wizara ya Kilimo bali wizara ya Ulinzi.

Tunaamini kuwa pasipo maelezo ya kutosha kuna kitu kinafichwa,kijarida chako cha Cheche kinatarajia kukupatia taarifa wiki ijayo. Na tunaamini kitu hicho hakistahili kufichwa kwani kinahusu TAIFA LETU.

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Picha ya Mwaka



Aliyekuwa afisa wa BoT ambaye amehusishwa na kesi za EPA Bw. Amatus Liyumba alipofikishwa kizimbani.

JIUNGE NA WANAKIJIJI WENZAKO!

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia sisi!

KATUNI ZA WIKI





KUTOKA KWENYE MTANDAO

Akizushiwa mtu mtaani kuwa kaua albino halafu watu wakamuua, baadae ikagundulika hakuna albino aliuwawa, nani atarudisha uhai wa mtu huyo?—**Zitto Kabwe**

Kama mwandishi wa habari wa BBC aliweza kujitoa mhanga kupata taarifa na akazipata. Iweje nchi yenye vyombo vya usalama ishindwe kupata taarifa za wauaji, waganga na wanunuzi? - **William**

Kwa hiyo, tutarajie danadana nyingi kabla suala hili halijachukua mkondo wa kuridhisha. nadhani wanachofanya sasa hivi ni maandalizi ya kuhakikisha kuwa hata kama linafikishwa mbele, wakubwa hao wataendelea kuhifadhiwa bila madhara makubwa.—**Mpita Njia**

kwani wewe ni mwanajeshi? hayo ni mambo ya kijeshi wewe unataka ujue ili iweje. Mbona waajabu hivi wewe. Unataka kujifanya unachunguza mpaka siri zandani ya jeshi? Ingekuwa ni mahusiano ya kijeshi na marekani ungehoji? Au kwa sababu ni Iran? mbona mara kwa mara tunasikia tz wanashirikiana kijeshi na nchi za ulaya mbona hua huhoji, huu kama si umbeya ni nini? - **tz**

Unajua hapa nionavyo mimi Waziri alijua anachokisema ili kujaribu kuficha ukweli, ila vyombo vya habari vya wenzetu vimemuumbua. Ila ninacho wa tahadharisha ni kuwa kuikumbatia Marekani upande mmoja na Iran upande wa pili kuna madhara yake.—**Rchasemwa**

Hoja yao kubwa sasa (Chadema), ni ufisadi, wanasema CCM mafisadi na kila tukipita na nguo zetu za kijani wanasema mafisadi haooo...Tuwaombe wanachama na wakereketwa wetu wakatae kuitwa mafisadi – **Yusuph Makamba**

Soma Bure
hoja zenye nguvu

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: Mhariri@klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

Kanusho: ***Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.***